Women Enterprise Fund

MKATABA WA HUDUMA WA HAZINA YA WANAWAKE WAFANYABIASHARA

Mkataba wa huduma wa hazina ya wanawake wafanyabiashara (WEF) inaonyesha ahadi yetu ya kutoa huduma za ubora wa juu kwa wadau wote. Sisi katika WEF tunajitahidi kukidhi na kuzidisha matarajio ya wateja wetu wote na tumeainisha ahadi yetu kwa mwanamke wa Kenya.

Maono:
Hazina ya kudumu ya Kuwawezesha Wanawake wa Kenya kwa Maendeleo ya Kiuchumi na Jamii.

Dhamira:
Kuwezesha wanawake kiuchumi na kijamii kwa kutoa nafasi ya kupata mikopo, ujenzi wa uwezo, kuwaunganisha na masoko, miundombinu ya masoko, na biashara ya kitaifa na kimataifa kwa kupitia ubunifu kiteknolojia.

Maadili ya Msingi:
· Uaminifu · Utaalamu · Utofauti
· Usawa na Haki · Uwazi na Uwajibikaji
· Ushirikiano · Ubunifu
, Kazi ya Pamoja na Ujumuishi

Maagizo ya Msingi

1. Kutoa mikopo nafuu kwa wanawake wanaofanya biashara ili kustawisha biashara zao
2. Kuimarisha uwezo wa kibiashara wa wanawake na mashirika yao ili kuwawezesha kusimamia biashara pamoja na kuwapa maarifa ya kibiashara
3. Kusiaidia biashara zinazomilikiwa na wanawake ili kuimarisha uhusiano na makampuni makubwa ya kibiashara kupitia kwa kukadiria ubora wa bidhaa zao, ukuzaji wa bidhaa na ushirikiano.
4. Kusiaidia katika kupata mauzo ya bidhaa na huduma zinazozalishwa na wanawake wafanyabiashara Kitaifa na Kimataifa
5. Kuhamasisha na kusaidia uimarishaji wa miundombinu katika biashara ndogo ndogo kama vile masoko ya kibiashara au ukuzaji biashara utakaokuwa na faida kwa wanawake wafanyabiashara

MATRIX YA MKATABA WA HUDUMA WA HAZINA YA WANAWAKE WAFANYABIASHARA (WEF)

Na.	SHUGHULI/ HUDUMA INAYOTOLEWA	MAHITAJI	GHARAMA YA WATUMIAJI	RATIBA YA MUDA
1.	Kujibu Simu (simu ya mezani [landline] au yoyote rasmi)	• Simu	Bure	Sekunde kumi na tano (15).
2.	Kujibu maswali ya wateja wanaofika ofisini.	• Fika ofisini na uulize	Bure	Dakika moja (1)
3.	Kujibu barua	• Mawasiliano yaliyoandikwa (barua)	Bure	Siku tano (5) za kazi
		• Barua pepe na mitandao ya kijamii (Twitter, Facebook & Youtube)	Bure	Siku moja (1) ya kazi
4.	Kujibu malalamiko na shida za wananchi	• Toa malalamiko	Bure	Siku moja (1) ya kazi
5.	Kusuluhisha malalamiko	• Malalamiko kwa mdomo au kwa maandishi	Bure	Siku thelathini (30) za kazi
6.	Usajili wa wauzaji	• Fomu ya maombi iliyojazwa ipasavyo • Wasifu wa Kampuni • Cheti cha Kujiunga/Kusajiliwa • Cheti cha PIN • Cheti cha kuzingatia Ushuru /Cheti cha Misamaha (Exemptions) • Taarifa asilia ya benki • Nakala ya cheti cha usajili na mashirika husika ya udhibiti • Risiti ya malipo ya ada isiyorejeshwa • Nakala za fomu za kurejesha kila mwaka zilizojazwa na msajili wa kampuni • Kitambulisho/pasipoti • Cheti cha AGPO (Kulingana na kategoria inayotumika panapohitajika) • Cheti cha Ulemavu (Kulingana na kategoria inayotumika panapohitajika	Bure	Siku kumi na nne (14) za kazi
7.	Utayarishaji wa zabuni	• Wasilisha zabuni kwa ajili ya bidhaa na huduma	Bure	Siku tisini (90)
8.	Kutangaza walioshinda na walioshindwa zabuni	• Ingia kwenye e-procurement kwa tangazo	Bure	Siku moja (1)
9.	Malipo ya bidhaa na huduma zilizopokelewa	• Wasilisha ankara/barua ya uwasilishaji/Nakala ya LPO/LSO na maelezo ya Benki yaliyotiwa saini ipasavyo	Bure	Siku sitini (60)
10.	Kutupa bidhaa zisizohitajika/za zamani	• Uwasilishaji wa zabuni	Bure	Siku sitini (60)
11.	Ushiriki wa umma katika mchakato wa kutengeneza sera	• Kujifahamisha na masuala, na ushiriki amilifu	Bure	Siku moja (1)
12.	Kuajiri wafanyakazi	• Tuma maombi rasmi kulingana na tangazo	Bure	Siku tisini (90) za kazi
13.	Utayarishaji wa maombi ya Habari	• Ombi la Habari	Bure	Siku ishirini na moja (21)
14.	Ujenzi wa Uwezo	• Ni lazima kiwe kikundi cha wanawake kilichosajiliwa	Ada ya mafunzo Kshs.100 kwa kila mwanachama	Siku saba (7) za kazi baada ya kupokea ombi la mafunzo.
15.	Kuziunganisha biashara za wanawake na mashirika/makampuni makubwa kupitia mafunzo, maonyesho au nafasi za mtandao.	• Lazima iwe biashara inayomilikiwa na wanawake na ambayo imeonyesha nia ya huduma hizo. • Uwepo wa fursa za kuunganishwa.	Gharama inagawanywa kati ya mnufaika na WEF.	Gharama inagawanywa kati ya mnufaika na WEF.
16.	Msaada wa soko kupitia maonyesho, majukwaa ya biashara mtandaoni miomgoni mwa mengine.	• Uwepo wa nafasi za kusaidia kupata soko • Biashara iliyosajilishwa na inamilikiwa na wanawake • Inazalisha bidhaa na huduma zinazotumika katika masoko ya kitaifa na ya kikanda • Kujiwekea mipango yao ya usafiri wenyewe	Gharama inagawanywa kati ya mnufaika na WEF.	Siku kumi na nne (14) za kazi baada ya kupokea maombi.

TUMEJITOLEA KWA ADABU NA UBORA KATIKA UTOAJI WA HUDUMA

Huduma yoyote ambayo haitekelezwi kulingana na viwango au afisa yeyote ambaye hatendi kazi kulingana na Mkataba wa Hudumakwa wananchi inapaswa kuripotiwa kwa:

Afisa Mtendaji Mkuu (Chief Executive Officer)
Women Enterprise Fund, Ghorofa ya 11, Jumba la Britam Tower, S.L.P. 17126 - 00100 NAIROBI;
Simu: 0714606845/6,
Simu ya dharura: 0793324820;
Barua pepe: complaints@wef.co.ke
Tovuti: www.wef.go.ke

Katibu wa Tume (The Commission Secretary) / Afisa Mtendaji Mkuu (CEO), Tume ya Haki za Utawala (Commission of Administrative Justice),
Ghorofa ya 2, West End Towers, Mkabala wa Shule ya Upili ya Aga Khan kwenye Waiyaki Way – Westlands, S.L.P. 20414- 00200, NAIROBI.
Simu: +254-20-2270000 / 2303000 / 2603765 / 2409574 / 0777 125818/ 0800221349 (Bila malipo)
Barua pepe: info@ombudsman.go.ke

KILA RAIA ANA HAKI YA KUPATA TAARIFA

Ukimwezesha mwanamke, unawezesha Familia na Taifa zima